



## CATHOLIC SECRETARIAT

TANZANIA EPISCOPAL CONFERENCE

P.O BOX 2133  
PHONE 022/2851075-7-8  
022/2850047  
022/2850017  
FAX 022/2851133; 2850427  
DOMAIN: TEC.CO.TZ  
E-Mail: [info@tec.or.tz](mailto:info@tec.or.tz)  
DAR ES SALAAM  
TANZANIA

*Department:* LITURGY

*Reference:* TEC/MED/32/3

Machi 19, 2020

### **YAH: SALA DHIDI YA JANGA LA VIRUSI VYA CORONA**

Ee Mungu Baba Mwenyezi, / Muumba wa Mbingu na dunia, / ulimwumba mwanadamu kwa sura na mfano wako / na kumpa mamlaka ya kuutawala ulimwengu huu, / **(Mwa. 2: 7-8)**. Tena Kwa upendo wako ulimtuma Mwanao ulimwenguni / kumkomboamwanadamu dhaifu / kutoka utumwa wa dhambi na mauti / na kumjalilia ahadi ya uzima wa milele, **(Yoh.3: 16)**. Naye alimtuma kwetu Roho wa haki na kweli / ili atukumbushe yote ambayo Kristo alitufundisha, / yaani kukujua Wewe Mungu wa kweli / na kukutumikia siku zote za Maisha yetu, **(Lk.24:49)**

Tunakuja mbele yako kwa unyenyekevu mkubwa, / tukitambua udhaifu wetu na kukiri dhambi zetu mbele yako. / Tunaomba msamaha maana tumekukosea Wewe Mungu, / uliye mwema na mwenye haki, / **(Zab. 51:3-4)**. Tunayo matumaini makubwa kwako Mungu Baba wa milele, / kwa kuwa kamwe hukuwaacha wanadamu peke yao katika mahangaiko, / bali uliahidi kuwasaidia na kuwarudishia matumani, / maana ulisema / "Mimi

nitawasikiliza kutoka juu mbinguni; / nitawasamehe dhambi yao na kuisitawisha nchi yao," (2 Nya7:14).

Kwa matumaini hayo, / Ee Baba wa Mataifa yote, / tunakuomba kwa wema wako / utuepushe na janga hili la ugonjwa unaotokana na virusi vya Korona. / Tunakuomba uwaponye wagonjwa wote / kwa mkono wako wenye nguvu na matumaini. / Uwakinge watu wa Mataifa yote / wasipate na maambukizi mapya ya ugonjwa huu, / ambao hadi sasa hauna tiba wala chanjo. / Uwajalie Wanasayansi na Watafiti ulimwenguni, / mang'amuzi sahihi ili waweze kupata chanjo na tiba ya ugonjwa huu.

Tunaomba hayo / kwa njia ya Kristo Bwana wetu. / Amina Mama Bikira Maria, / Salama ya wagonjwa, / na mlinzi wa Taifa letu. Utuombee.

Imeidhinishwa na

+ 

+ Salutaris Libena



**MWENYEKITI WA IDARA YA LITURUJIA (T)**